



Passionately Tanzanian

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KUITAMBULISHA WIKI YA KIKOA CHA DOT TZ

NDUGU WANA HABARI,

Utangulizi

Kikoa cha dot tz au dot tz domain name kwa kiingereza, ni rasimali muhimu kwa taifa letu katika mawasiliano ya mtandao wa Intaneti. Dot tz inatumika kwa ajili ya upatikanaji wa taarifa muhimu kupitia tovuti (website) na mawasiliano ya kielektroniki yaani baruapepe (e-mail). Kikoa hiki kinawezesha sekta binafsi na za umma, katika utoaji wa huduma na kufanya biashara nchini na kimataifa kupitia mtandao wa Intaneti. Ni utambulisho mahususi usio na shaka katika mawasiliano ya mtandao kuwa mtoa huduma au mfanyabiashara anayetumia kikoa cha .tz anatoka Tanzania. Matumizi ya .tz zaidi ya utambulisho mahususi ya Utanzania, yanamhakikishia mtumiaji wa kikoa cha dot tz usalama mtandaoni na vilevile yanapunguza gharama za mawasiliano. Dot tz inawezesha mawasiliano kubakia ndani ya mipaka yetu na hivyo kuharakisha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha usalama wa mawasiliano yetu.

Rajisi ya dot tz ndio kampuni iliyokasimiwa kisheria kuendesha mitambo inayoifanya dot tz ipatikane kwenye mtandao tangu mwaka 2009. Rajisi hii inafahamika kama Tanzania Network Information Centre (TZNIC). Kutokana na ukweli kwamba rasilimali hii muhimu ya kikoa cha dot tz yenye manufaa yalioainishwa hapo juu hakijaweza kutumiwa na watanzania wengi ipasavyo (*Kwa mujibu wa takwimu mpaka sasa tuna vikoa takribani 13,800 vilivyosajiliwa ukilinganisha na watanzania zaidi ya milioni 20 wanaotumia mtandao wa Intaneti*), Uongozi wa rajisi ya dot tz umeonelea ni muhimu kuanzisha maadhimisho ya wiki ya kikoa cha dot tz . kila mwaka, katika wiki moja ya mwezi Juni kuanzia mwaka huu 2017.

Wiki ya Kikoa cha Dot tz.

Tunapenda kuwatambulisha kuwa, maadhimisho ya wiki ya kikoa cha dot tz kwa mwaka 2017 yataanza rasmi tarehe 12 Juni hapa Dar es Salaam na kilele chake kuazimishwa 15 Juni huko Dodoma.

Kauli mbiu ya wiki ya kikoa cha dot tz kwa mwaka huu wa 2017 ni “ **.tz kwa usalama na utambulisho mtandaoni**”.

Katika wiki ya kikoa cha. tz mwaka huu ,rajisi ya .tz kwa kushirikiana na mawakala wake itatoa elimu juu ya faida za matumizi ya vikoa vya dot tz kwa umma na wadau mbali mbali kupitia vipindi vya runinga na redio nchini. Tarehe 12 Mwezi Juni rajisi ya kikoa cha .tz itaendesha semina ya elimu ya vikoa vya dot tz kwa umma na kwa wadau hapa Dar es salaam, katika hoteli ya New Africa. Mnamo tarehe 15 Juni huko Dodoma patakuwa na kilele cha maadhimisho ya wiki ya kikoa cha .tz ambapo kutakuwa na uzinduzi rasmi wa tovuti ya www.karibu.tz. Inayotarajiwa kuzinduiwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tovuti hii ya www.karibu.tz itamuwezesha kila mtanzania ,mfanyabiashara na mtoa huduma kujipatia huduma ya kusajili moja kwa moja kikoa cha dot tz kupitia mawakala walio idhinishwa na rajisi ya .tz, ambao wameunganishwa katika tovuti hii.

Wito

Rajisi ya kikoa cha dot tz inatoa wito kwa wanahabari , watanzania na wadau wetu wote kutega sikio katika runinga na vipindi vya redio ili kujifunza zaidi faida za kusajili na kutumia vikoa vya .tz. Aidha, Mawakala wetu walio idhinishwa kusajili vikoa vya dot tz ambao ni wadau wetu muhimu katika usajili wa vikoa vya dot tz watashirikiana bega kwa bega na rajisi ya dot tz kutoa elimu kwa umma pamoja na kusikiliza na kutatua kero mbali mbali za wasajiliwa wa vikoa vya dot tz pamoja na kusajili vikoa vipya vya dot tz.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na rajisi ya dot tz kupitia:-

Simu: +255 22 2772659

Baruapepe: info@tznictz.or.tz

Tovuti: www.tznictz.or.tz

Facebook: www.facebook.com/tznictz

Twitter: www.twitter.com/tznictz

Instagram: www.instagram.com/tznictz

Youtube: www.youtube.com/tznictz

Ahsanteni.

Imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji ,Rajisi ya .tz